# Mama Frances Streitel

## Mwanzilishi wa Shirika la Masista wa Mama wa mateso



# Mama Frances Streitel

## Mwanzilishi wa Shirika la Masista wa Mama wa Mateso



Sisi Masista wa Mama wa mateso, tunapenda kushiriki nawe zawadi Mungu alizotujalia sisi na Kanisa, kupitia Mama Frances Streitel mwanzilishi wa shirika letu la kitawa.

Mara nyingi tunajiuliza huyu mwanzilishi ni nani? Alifanya nini wakati wa uhai wake? Na ipi ni karama yetu? Kwa sababu hiyo tunawaleteeni jarida hili ili muweze kujifinza Kwa urahisi historia ya Mama Frances na karama maalumu aliyojaliwa na Mungu Roho Mtakatifu.

Kwa pamoja Turudi nyuma na kuangalia hatua muhimu katika maishaa yake, na kwa undani kufahamu maarifa yake katika kumjua Mungu, na vipi yalimwongoza katika njia ambayo daima haikuwa rahisi. Nguvu ya Mama huyu hasa ilipatikana katika imani ambayo daima ilimwongoza kufuata mapenzi ya Mungu na matakwa yake. Alikuwa kama bibi arusi katika wimbo ulio bora, hakuweza kupata amani hadi ampate mpendwa wake..Maisha na matendo ya Mama Frances tunaweza kuyaweka kwa kifupi katika maneno yafuatayo : *„Furaha yangu ya juu – na iwe katika kutimiza wajibu, na kutekeleza Matakwa ya Roho wa Mungu anipendezae."* [1]

Tuangalie maisha yake kwa kufuata hatua zake…

# MWANZO KAMA
# WALIVYO WENGINE WENGI

Mnamo tarehe 24 Novemba mwaka 1844, wazazi wake Adamu na Franziska Hörhammer Streitel walifurahia kuzaliwa kwa kifungua mimba wao Amalia. Alizaliwa Mellrichstadt, Ujerumani. Picha ya eneo la mraba wa mji yaonyesha kuwa mji huo uko katika mwambao chini ya mlima Thon na msitu wa Thuringian. Kutokana na desturi ya wakati wake alibatizwa siku ya kuzaliwa nyumbani kwa wazazi, na kuitwa jina *Amalia Frances Rose*.



Wazazi wake walioshi Imani thabiti ya dini ya Kikatoliki, walikuwa na watoto wengine watatu: Adamu, Hermann na Hedwig.



Familia ya Streitel ilidhihirisha kweli upendo kwa Mungu na Jirani kwa kuwapenda masikini, wagonjwa na wahitaji, kwa pamoja wakaifanya familia yao kuwa mfano bora wa imani ya kikatoliki, ambapo kila siku walisali,wakahudhuria Misa Takatifu na kuadhimisha sherehe za kanisa hasa zilizomuhusu Mama Bikira Maria kama msingi madhubuti.

# UTOTO WAKE

Kutokana na akili kamili aliyokuwa nayo, na Tabia yenye moyo wa uchangamfu, Amalia kwa haraka alijifunza Kujizuia na Kujiheshimu, kutokana na malezi ya mama yake ambae alikuwa mtii, asiyepoteza wakati na mwenye utaratibu katika maisha yake ya kila siku.

Katika umri wake wa mwanzo alifundishwa kufanya kazi za nyumbani akawa hodari katika ushonaji. Alifundishwa pia kwa makini jinsi ya kuwa mwema katika jamii kulingana na kiwango cha ushirikiano uliokuwepo katika familia. Kushiriki wajibu mbali mbali kulimfanya aishi maisha ya faragha ambayo yalikuwa ndio hamu ya moyo wake.



# ROHO KWA AJILI YA MUNGU

Malezi ya kidini kwa Amalia yalianza Tangu utoto wake. Alipokuwa mwenye umri wa miaka miwili alifundishwa na Mama yake kupiga ishara ya msalaba na kusali sala fupi. Hakuwa mashuhuri kiakili tu, isipokuwa aliwapenda pia watoto masikini waliomzunguka. Upendo kwa jirani, na upendo wa kweli kwa Mungu, vilikua kutoka ndani, hali iliyomfanya ajitambue mara kuwa anaiatwa kuishi maisha ya kitawa.



Alipokuwa mwenya umri wa maika tisa alivutwa kufahamu maneno ya Kristu yasemayo *"Nami nitakapo inuliwa juu ya nchi, nitamvuta kila mmoja kwangu."* [2]

Kwa kupokea Komunio ya kwanza mnamo tarehe 9 april 1857 kulimfanya aunganike zaidi na Mungu na kuwa imara.

Tabia nyingine muhimu ya utu wake na malezi yake ya kikristu ni mapendo ya dhati kwa Mama Bikira Maria, ambayo ni malezi ya familia na uwepo katika mji wake wa baadhi ya kumbukumbu muhimu kwa Mama Bikira Maria wa Mateso.

# UJANA WAKE: MUDA WA KUSEMA "NDIO"

Baada ya kumaliza elimu yake ya msingi Amalia alitumwa kwenda Augsburg Ujerumani, kwenye chuo cha Wafranciskani kijulikanacho kama *Maria ni nyota* ambako alimaliza mafunzo yake na kutunukiwa cheti cha Stashahada kwa masomo ya kifaransa na Muziki.



Mnamo Tarehe 24 Septemba 1857 alipokea Sakramenti ya Kipaimara, iliyomtia nguvu ya kujitambua kuwa alikuwa anaitwa kuishi maisha ya kitawa. Namna ya kuitwa kwake kwenda kuishi maisha ya kitawa, haikujulikana kwa Amalia. Baadae mwenyewe alisimulia kuwa, hadi alipotambua njia hiyo ya pekee alikuwa mwenye umri wa miaka kumi na Saba. Katika kitabu chake cha kumbu kumbu mbali mbali,yaonyesha kuwa mnamo mwaka 1862 aliitwa kwenda utawani.

Wazazi wake walipinga sana uamuzi wake wa kuingia utawa, walipendelea aolewe. Hali hiyo ya kusikitisha ilifikia kikomo baada ya kuivumilia kwa muda wa miaka minne, na siku moja alijificha kwenye dari myumbani akikataa kutambulishwa kwa wanafunzi wanasheria, kama uwezekano wa kupata mchumba. Kwa jinsi hiyo Amalia alionyesha nia yake, na kujibu Mwaliko wa Bwana, wa kuishi maisha ya kujitoa kwake tu.

# Matakwa yake yanatimia kweli

Mnamo tarehe 25 Septemba 1866 Amalia aliingia Maisha ya utawa katika chuo cha Wafranciskani Kiitwacho Maria ni nyota alipojifunza wakati wa ujana wake. Wazazi wake walikuwa wamemruhusu kwa mashariti kwamba konventi anayoingia isiwe ya mashariti magumu yaani maisha ya ndani, wala wanaojihusisha na kutunza wagonjwa. Lakini Amalia alimwambia mara Mama mkubwa maelekeo yake kwamba ni kutunza waganjwa. Badala ya kukubali mapendekezo yake, aliombwa aendelee na mafunzo yake ambayo ni kifaransa na muziki.



Aliingia Unovisi mnamo tarehe 3 Juni 1867 na kupewa jina la sista Angela, na kufunga nadhiri zake za kwanza baada ya mwaka mmoja.

Ingawa nia yake ya kujiweka wakfu ilitimia, alikuwa bado akipambana kwa sababu alipendelea malezi ya kidini yaliyo makali na magumu. Alijiweka katika hali ya kutii, ambapo aliombwa kufundisha na baadae aliteuliwa kuwa mama mkubwa. Baada ya muda Sr. Angela aling'amua kwamba anapaswa kuacha jududi yake ya mwanzo ya mazoezi makali ya kujinyima, na kuanza kuishi maisha mepesi ya kujinyima yasiyo makali kama mwanzo. Ugonjwa mkali uloihitaji sadaka ya kulala kitandani kwa muda wa wiki tano, kwenye godoro la mwani



(aina fulani ya majani ya majini) kulimpatia utamabuzi wa ndani katika maisha yake. Hali hiyo ilimafanya abadili mtindo wa maisha ya kitawa aliouanza mwanzo, na kufuata mtindo mwingiine wa waisha ya kitawa alioanzisha mwenyewe, ambapo alipigana vita vikali dhidi ya upenda wake.

Alichotaka hasa kufanya ni kujizoeza kuishi ufukara kama wa Mtakatifu Francisko wa Assizi.Hali hii ilimafanya ajiweke upya, siyo tu katika maisha ya kitawa, isipokuwa hata kwa kanisa na jamii. Tena alijumuisha nafasi muhimu na kuacha yote yasiyo ya lazima. Alipenda mwenyewe kufanya kazi alizopangiwa, na kuongoza sala za kina ndani ya moyo , daima akabaki chini ya mwangaza wa pendo la Mungu. Kwa jinsi hiyo alikuza hamu ya kuishi kadiri ya mfumo asilia wa kanuni ya Mtakatifu Franciscko wa Assizi. Na kwa nguvu alitambua wito wa kuishi mtazamo wa ufukara kiroho, na katika mali na kuupenda msalaba ndani ya kanisa, na Ulimwengu mzima.



# Conventi ya Wakarmeli



Kutokana na matunda ya maisha ya sala Sr. Angela alitambua wazi kwamba anahitaji kwa kina kuunganika na Mungu, sala ilikuwa ndio njia pekee ya kumpatia nguvu. Kwa njia ya sala alitambua kwamba Mungu alikuwa ananwita katika njia mpya, kwa sababu hiyo aliomba kuacha Chuo cha *Maria ni nyota* na Kuingia Conventi ya Wakarmeli wa *Mlango wa Mbingu* huko Ujerumani. Uamuzi huu wa kuondoka katika Chuo cha *Maria ni nyota* na kuingia Conventi ya Wakarmeli mnamo tarehe 25 Januari 1882, kulimuweka katka mapambano ya ajabu ya ndani.

Mara baada ya kuingia Conventi ya Wakarmeli alipokea vazi la Unovici na kupewa jina "Sr. Petra". Hapo Carmeli alianza hatua mpya ya maisha. Bwana alimjalia neema tena ya kuanza safari kuelekea kwake.

Mojawapo kati ya barua zake aliandika, *"Niliingia Carmeli kwa njia ya Sala na sadaka mahali nilipopatafuta kwa muda mrefu.Nipata Unovici, nikapaswa kuwa mtii. Mara nyingi nilipata wasaa wa kujishusha wakati wa kipindi cha miaka kumi ya uongozi wangu. Tena nilikuwa kama mtoto, Roho yangu ikawa karibu na Mungu."* [3]

Sr. Petra mara kwa mara alijitoa kabisa kwa Mungu. Mara akajikuta katikati ya jangwa ambapo Sauti ya Mungu ilikuwa wazi kwa Roho yake.

# WITO MPYA:

## *Tafakari na kazi: njia nyepesi.*

Pale Carmeli walijishuaghulisha kusali na Ukimya.Sr. Petra alitambua kwamba Mungu hakumwita katika maisha ya ndani, bali aunganishe maisha ya sala na kazi katika shirika jipya la kitawa atakalo lianzisha. Mang'amuzi yake hayo ya ndani (moyoni) yalimfanya aache myumba yake ya Utawa wa wakarmeli na kuwa tayari kufanya kazi mpya aliyopewa na Mungu. Haya ni yale aliyoyaandika kuhusu wito wake wa kuishi Karama ya pekee ambayo ingeunganisha mambo haya mawili pamoja; maisha halisi ya utendaji na maisha ya Sala na fikara.

*"Nilikuwa nasali kanisani kabla ya mchana, nikaona kitu fulani ambacho ni kigeni kabisa kwangu. Katika maono yangu, kulikuwa na milima miwili imesimama. Milima hii ilisimama pamoja katika mstari. Mlima uliokuwa upande wa kulia ulikuwa mrefu zaidi kuliko ule mwingine na ulikuwa na namna*





*fulani ya ngazi. Kwenye kilele cha mlima huo, naamini nilimwona mtakatifu Eliya katika namna ya ajabu, na halafu chini ya mlima huo nilimuona Mtakatifu Teresia. Mlima huu Mwingine haukuwa mrefu sana, inawekana kwa sababu haukuwa na miaka mingi. Mlima mmoja, niliutambua kuwa ulikuwa mlima karmeli na Mwingine ulikuwa Alverna ambapo mtakatifu Francisko alikuwa amesimama, akiwa ameshika msalaba mikoni Mwake.Milima yote miwili ilielekeana na kukutana pamoja, ule mrefu ulielekea kupinda na kukutana na ule mwingine, mahali ambapo alikuwa amesimama Mtakatifu Teresia......*

*Wito ambao niliupokea kabla kutoka kwa Mungu au ule nilioupata baada ya maono haya, sikuweza kuuelewa na hivi nilijiuliza, kwa nini Mungu anataka kuniondoa tena huko Karmeli? jibu likasikika hivi: "Unganisha pamoja maisha ya kiutendaji na maisha ya Sala na fikara." Pengine hili lilitoa Mwanga kwa yale niliyoyaona. Karmeli ingeweza kuwakilisha sala, na Alverno inawakilisha kazi. Mambo yote mawili Sala na kazi yamepata mielekeo na thamani mpya kadiri karne zilivyopita, ambapo Kabla yake, mara nyingi Viliwakilishwa visivyo kwani kitu kimoja au Sala ilionekana kuwa bora zaidi na ya lazima zaidi kuliko kazi, au kazi ilionekana kuwa bora zaidi na ni muhimu zaidi kuliko sala. Katika shirika ilikuwa vigumu kuelewa daima au kutofautisha kati ya "Sala ya kazi"; na "kazi ya Sala" Sala na kazi ni lazima viende pamoj kama watoto mapacha, vikijitahidi Kuondoa mateso na matatizo ya mwanadamu kiroho na kijamii, ikiwa inafundisha tena maana na umuhimu wa kusali na kufanya kazi."*[4]



*" Kwa imani Abrahamu aliondoka kutoka kwenye nchi yake na kwenda mahali pengine, bila kujua aliko kuwa anakwenda"* (HEBR 11)

Mungu alimwonyasha Sr. Petra, lengo lake tena wakati Padre Fransisko Jordano alipomwomba Sr. Petra kushirikiana naye katika kujenga na kuimarisha tawi la akina Mama la taasisi yake mpya, likiwa na lengo la kutoa elimu ya kikristo. Kama vile Abrahamu kwa imani na utii kwa mapenzi ya Mungu, Sr. Petra aliondoka kwenda Roma bila Kujua bayana alichokuwa anakwenda kukifanya. Kama Bikira Maria alivyosema Ndiyo kwa malaika Gabriel ndivyo Sr. Petra alivyofanya, bila kujua Mungu anakompeka na anachokwenda kufanya.



Mnamo tarehe 16 Februari 1883, Sr. Petra aliwasili mjini Roma tayari kuanza kazi mpya katika Kanisa. Upendo wake katika ufukara na Kanisa, alivionyesha katika makazi yake ya kwanza aliyoyachagua kwa ajili ya Masista, yaliyo jirani na eneo la Mt. Petra eneo



lililo tupu  lisilo na mapambo. Mwanzoni nyumba haikuwa na kitanda wala kiti isipokuwa baadhi ya vifaa vya jikoni. Utume mpya wa Bwana alioaminishwa ulimfanya achague jina Jipya: Sr. Maria Frances wa Msalaba.

Kwa muda wa miaka miwili Sr. Maria Frances na Padri Jordani walifikiri kushirikiana kutokana na ugumu na kutoeleweka kwa karama mbili tofauti kati yao kwa Sababu zote waliziamini. Kwa sababu hiyo kutengana hakukuzuilika. Kasisi mwenye madaraka alitenganisha chuo kilicho ongozwa na Maria Frances Kutoka kwa kile kilicho ongozwa na padri Jordan (Jumuia ya Mungu Mwokozi, ijulikanayo kama Wasalvatoriani)

# Masista wa Mama wa Mateso wa kanuni ya utawa wa tatu wa Mtakatifu Francisko wa Assizi

Shirika la Masista wa Mama wa Mateso lilianzishwa na Sr. M. Frances akiwa mwanzilishi na Mama mkuu. Tangu wakati huo na kuendelea anajulikana kama Mama Frances.

Jumuiya mpya kwa uangalifu ilifuata kanuni ya Mtakatifu Francisko na kwa namna ya pekee waliishi ufukara wakigawana walichonacho pamoja na masikini.Ili kujikimu na maisha, Masista walikuwa na bidii katika kufanya kazi mbali mbali, kama kuhudumia wagonjwa katikanyumba zao, na kutunza Sakristia katika kanisa la Camposanto Teutonico lililo Vatican. Masista waliishi kama watu masikini kati ya masikini. Wakifuata na kutafakari juu ya Kristu na Mama Maria akiwa chini ya msalaba. Sakramenti na Liturgia ya saa Takatifu vilikuwa ni chakula chao. Walifanya kila waliloweza ili watu watakaokutana nao waweze kumuona Mungu kupitia tabasamu katika nyuso zao, maneno ya kutia moyo, na wema katika kuwakumbatia wote.



Jumuia ilikua, na kuongezeka kwa wanachama

kulilazimisha jambo jipya, kwanza kabia katika hitaji la chakula kwa vile Masista waliruhusiwa kukusanya masikini. Baadhi ya Masista walitoka Ujerumani, Austria, Ufaransa na Poland. Wengine walitoka U.S. Amerika na kuwasili Kansas mnamo mwaka 1888 kuomba Sadaka, Lakini walikuta ufukara kiroho na hata katika vitu, ambapo kupitia maombi ya kasisi mwenye madaraka katika oneo lile, waliruhusiwa kuishi wakitunza wagonjwa na masikini. Walikwenda kwa nia ya kupokea, lakini bado walijukuta wakitoa.


Kwa kuwa mwaminifu katika kazi yake, Mama Frances alipokea kila kitu kutoka mikononi mwa Mungu. Ingawa baadae alipata Maumivu na Msalaba wakati alipoandolewa Madarakani na kwenye ofisi ya Mama mkuu akiwa kama kiongozi, kwa sababu ya mambo fulani fulani kutoeleweka. Alisaidiwa na ukweli kwamba kila kitu ni chema kwa sababu kimetokea kwa ruhusa ya Mungu. Aliishi mwaka wa mwisho wa maisha yake kwenye nyumba yenye boma iitwayo Sant Elia, Provinci ya Viterbo Italia akihudumia watoto katika shule ya Chekechea,kutoa huduma kwa wagonjwa, na kutenda yaliyo bora kwa moyo wa kimama kati ya Masista wenzake.

Baada ya muda kupita alifariki mnamo tarche 6 Marchi 1911.

Katika siku hiyo hiyo Baba Mtakatifu Pius wa X aliidhinisha katiba ya Masista wa Mama Maria wa Mateso wa kanununi ya utawa wa tatu wa Mt. Francisko wa Assizi iliyotambulisha zawadi ya Roho Mtakatifu aliyopewa Mama Frances katika kuanzisha Shirika Letu. Alitembea katika njia hii kuelekea utakatifu, na ndivyo tufanyavyo na tuna matumaini kwamba na kizazi kijacho kitaedelea kufanya hivyo hivyo.

# Katika Moyo wa Mama Frances

Mama Frances alipata chakula cha kiroho kutoka katika maandishi ya Francisko na ya Wakarmeli, kwa namna ya pekee toka kwa Mtakatifu Francisko na mtakatifu Clara wa Assizi pia kutoka kwa Mtakatifu Tereza wa Avila. Alikuwa imara akivutwa na njia ya Watakatifu hawa watatu kwa sababu walipenda na kuthamini *utu wa Binadamu* na matakwa ya Mungu na si hivyo tu, bali wakawa na uwezo wa kuyaishi hayo.



Kutoka kwa Mama Frances "Ni wazi" ndio hapo lilipo chimbuko la jumuiya yetu, Masista wa Mama wa Mateso. Sote tunatambua kuwa zawadi za Mungu zinasitawishwa na mchango wa kila mmoja wetu, na kwa wale wote Mungu atakaowaita kushiriki busara na karama ya Mama Frances. Zawadi aliyopewa na Roho wa Mungu ya kumuita kuanzisha familia moja ya kitawa, tunaweza kuifupisha katika pointi fupi yenye maana kwamba chimbuko lake ni katika kuutafakari msalaba na Mama Maria akiwa chini ya msalaba.

## *Upendo kwa Yesu, Binadamu na Ekaristi*



Haya ni mambo mawili ambayo ni kiini kinachotokana na Roho ya Kifrancisko na ya Kikarmeli. Fumbo la Umwilisho na Ekaristi ndio alama ya juu kabisa ya upendo wa Mungu kwetu. Mwanzo Mungu alihiari kuchagua kushiriki ubinadamu wetu, maandishi yanatujulisha Maneno Maya. *"Nami nipo pamoja nanyi siku zote, naam mpaka mwisho wa nyakati."* [5]

Mama Frances hasa akielekea mwaka wa mwisho wa maisha yake, aliishi kwenye nyumba yenye boma iitwayo Sant' Elia, akitumia muda wake mwingi katika kusali. Kuabudu Sakramenti takatifu ndiko kulidhihirisha upendo wake kwa Yesu na Binadamu na kutamani kumtii Bwana. *"Bwana sitamani kitu chochote isipokuwa wewe, wewe tu napenda kukushika kabisa."* [6]



Kadiri ya Mama Frances pango la Mtoto Yesu na Msalaba vinapaswa kurudiwa tena na tena katika utajiiri wote wa Kiriho, kwa binadamu wa nyakati hizi, kwa kuwa ni alama wazi ya upendo wa Mungu usiogawanyika, na kwa njia hiyo Mungu alitupenda sisi, na akajitoa mwenyewe kwa ajili yetu.

## *Maria chini ya Msalaba*

Mama Frances na Masista wenzake walimtazama daima Mama Maria akiwa chini ya Msalaba kwa kuwa ndiye aliyekuwa kiongozi na kielelezo katika maisha ya kila siku. Roho ya Mama Frances iliguswa kwa utayari na uelekevu wa Mama Maria katika kufuata matakwa ya Mungu,anasema:

*"Kuchukua mzizi kwa Maria Immaculata, na kuunda sura yake ndani kutokana na kielelezo cha Mungu, kujulishwa nae Mafumbo ya upendo na mateso, hapo ndipo nitakapokuwa kweli bibi arusi wa Msulibiwa ambae kamwe hataweza kuniacha. Ee Damu ya Kristu iliyotona miguuni. Hadi mpendwa Msulibiwa atakaposema:"Njoo kuku juu chukua nafasi yako katika kiini cha moyo wangu".*[7]




Tukilinganisha uwezo wetu wa kutekeleza matakwa ya

Mungu kadiri ya mipaka yetu inaonekana kuwa ni vigumu.Hata hivyo Mama wa Mateso alitufundisha kuwa dhabiti bila kushurutishwa wala mashaka.

## *Upendo kwa Kanisa*

Kwa Roho ya Kifrancisko Mama Frances alitushirikisha upendo wake kwa kanisa. Ingawa alijua kuwa kanisa la wakati wake lilikabiliana na hali ngumu.



Hakuwa mtu wa hukumu, ila alipendelea Sana upya wa mtu ambao ulikuwa unaanza ndani Mwake au moyoni Mwake. Mama Frances alijua wazi kuwa alichokiona, kilikuwa ni Mapenzi ya Mungu, tena kingekuwa na faida kwa kanisa nzima duniani.

*"Sala yangu leo pangoni kwa Mwokozi katika altare iliyojuu ya fukara mtakatifu ni hii: Ee Bwana ulileteee kanisa lako enzi na heshima. Ulijalie kanisa lako, ili vazi lake la harusi lionekane katika weupe wa rangi zake mpya,rangi au fadhila ya unyenyekevu na rangi au fadhila ya ufukara. Kwa ajili ya utukufu wako, uwape nguvu na ari watoto na vijana ambao wanamoyo wa kukufuata Wewe katika maisha ya kujikatalia mambo ya kidunia, na kuishi kwa ukamilifu maisha ya kujikana, anaye jifanya mdogo, atakuwa mkubwa mbele yako Bwana".*[8]

## *Kupenda ufukara*

Kupenda ufukara ni moja kati ya misingi mikubwa ya maisha ya Mama Frances; aliwaza kuwa Kupenda ufukara ndio Mama wa fadlhila nyingine zote. Mama Frances na msista wenzake wa kwanza walichagua na kuishi maisha ya ufukara wa mali kwa uaminifu mkubwa. Wakati huo huo walichukua na kuishi kwa moyo,ufukara wa mali na wa roho wa watu wangi. Ni ufukara tu ndio unaweza kutufanya sisi, tuwe na moyo huru kwa ajili ya Mungu.

*" Oh Bwana, akujulishe katika alama zinazosikika za furaha ambazo zitatayarishwa kwa ajili yake, iwapo kizazi kipya fukara kitatokea kwa ajili yake. Kama roho ya asili ya dini, ikiamshwa tena katika moyo na dunia, lazima itambue kwamba amani ya kweli haitapatikana katika kumiliki utajiri wa dunia bali inapatikana na kujengwa katika kuka na utajiri na mali za dunia hii."* [9]



# Sisi, masita wa Mama wa Mateso, leo

Tukifuata nyayo za Mama Frances, tunamwangalia Bikira Maria aliye chini ya Msalaba wa Yesu Kama mfano halisi wa imani na ufuasi, na tunaishi roho ya Mtakatifu Francisko wa Assizi.Tunajaribu kutekeleza wazo kuu la Mama Frances katika kutafakari fumbo la Mungu kutokana na Hayo, mmoja anatafuta kuunganika na Mungu kwa kusali daima na kwa kuwa mtumishi aliyetayari kwa ajili ya kanisa na kwa ajili ya wale wote wanaohitaji msaada wa kimwili na wa Kiroho.







Tunakuwa makini  kwamba watu wengi walimdai Mama Frances na Masista wenzake nafasi ya kapata hali nzuri ya maisha kulingana na neno la Mungu, sisi pia tunatafuta  kuwa na hali nzuri katika kufanana na Ckristu.

Sisi Masista wa Mama wa mateso tunao Masista katika nchi zifuatazo: Austria, Kisiwani Caribbic Grenada, Jamuhuri ya Dominicani, St. Lucia, Trinidad, Brazil, Ujerumani, Italia, na Amerika.










Tunatoa huduma katika nyanja za Elimu Afya, Katekesi na kutangaza kuwa Mungu ni Bwana wa uzima. Kuanzia mwezi Julai mwaka 2006 kikundi kidogo cha Masista watatumwa kufanya utume katika jimbo la Kahama Tanzania Afrika.

Kwa kuishi maisha ya kujibidisha katika nyanja ya utume tukisaidiwa na Roho ya tafakuli, tunashughulikia wahitaji hasa masikini. Kwa uwezo wetu tunamtafuta Mungu zaidi ya vitu vyote.

---

1 Barua kwa wazazi wake na kwa dada yake Hedwig,barua ya 19(18)namba 5.Barua ya Mama Frances Streitel kwa mheshimiwa Joseph Joch barua ya 28(17) aya ya 2

2 Yohana 12:32

3 Barua kwa Padri John Jordan,barua ya 28(17) aya ya 6

4 Barua kwa Padri John Francis Jordan,barua ya 39(86) aya ya 8

5 Mathayo 28:20

6 Barua kwa Padri John Francis Jordan,barua ya 62(43) namba 3

7 Kutoka kwa Mama M.Frances kitabu cha kumbukumbu binafsi,tarehe 15 Decemba 1896

8 Barua kwa Padri John Francis Jordan.barua ya 75 (52) aya ya 2

9 Barua kwa Padri John Francis Jordan,barua ya 75 (52) aya ya 2

MCHAPISHAJI:
Éditions du Signe
B.P. 94 – 67038 Strasbourg – France
Tel: (0033) (0) 3 88 78 91 91
Fax: (0033) (0) 3 88 78 91 99
Email: info@editionsdusigne.fr
www.editionsdusigne.fr

MKURUGENZI WA UCHAPISHAJI: Christian Riehl

MKURUGENZI MSAIDIZI WA UCHAPISHAJI: Audrey Gilger

MAANDISHI: © Masista wa Mama wa mateso

PICHA:
© F. Zvardon: uk. 1 (mambo ya maisha yaliyokwisha pita), 4, 6 (maua), 7 (mambo ya maisha yaliyokwisha pita), 8, 9 (mambo ya maisha yaliyokwisha pita), 10, 11, 12, 13, 14, 15-16 (mambo ya maisha yaliyokwisha pita), 17, 18, 20, 21 na jarida.
© Heike Demarty-Ebeling: uk. 2 na 3 (mambo ya maisha yaliyokwisha pita).
© Masista wa Mama wa mateso: uk. 1, 3, 6, 7, 8, 9, 15, 18, 19, 22, 23, 24, yaliyo ndani ya jarida.

UBUNIFU NA UTARATIBU: Juliette Roussel

MSANII WA PICHA: Atelier du Signe (107083)

© Éditions du Signe, 2006
ISBN 13: 978-2-7468-1730-2
ISBN 10: 2-7468-1730-6
Haki zote zimehifadhiwa
Hairuhusiwi kunakiri
Kimechapwa Italia na Arti Grafiche

SUORE DELLA SS.MA MADRE ADDOLORATA
Casa Generalizia
Via Paolo III, 9
00165 Roma, Italia

REGIÃO BRASIL
CONVENTO MÃE DOLOROSA
Estrada Velha de Anápolis, km 06
Caixa postal 557
74001-970 Goiânia, GO
Brasil

REGION DEUTSCHLAND
Marienburg 5
D – 91183 Abenberg
Deutschland

REGIONE ITALIA
Via Longobucco, 19
00178 Capannelle, Roma
Italia

REGION ÖSTERREICH
Simmeringer Hauptstraße, 175
A – 1110 Wien
Österreich

US/CARIBBEAN PROVINCE
17600 E. 51st Street
Broken Arrow, OK 74012-9231